# SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

## MUHTASARI WA DINI
**KWA ELIMU YA MAANDALIZI ZANZIBAR**

**TAASISI YA ELIMU ZANZIBAR**

**2012**

© Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, 2012

Haki zote zimehifadhiwa, hairuhusiwi kuiga, kunakili, kutafsiri, kupiga chapa, maandishi nukta nundu na kutoa Muhtasari huu kwa jinsi yoyote ile bila ya idhini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Umetayarishwa na:
Taasisi ya Elimu Zanzibar
S.L.P. 840
**Zanzibar**

# YALIYOMO

**Ukurasa**

YALIYOMO ... ii
Utangulizi ... iii
Ujuzi wa Jumla wa Somo la Dini ... iii
Malengo ya Jumla ya Somo la Dini ... iv
MUHTASARI WA DINI KWA MWAKA WA KWANZA ... 1
MWAKA WA PILI ... 9

## DINI

# Utangulizi

Ukamilifu wa binadamu ni kuwa na tabia (akhlaq) nzuri. Kwa Muislamu misingi ya akhlaq inapatikana katika Qur – an na hadithi za Mtume (S.A.W). Kwa hivyo, ni muhimu mtoto apatiwe mafunzo ya tabia nzuri yanayotokana na Kur – an na hadithi za Mtume (S.A.W) tokea katika umri mdogo.

## Ujuzi wa Jumla wa Somo la Dini

Baada ya kusoma somo la Dini katika skuli za Maandalizi, watoto wataonesha ujuzi wa:-

1. Kufuata utaratibu mzuri wa kuishi katika jamii kwa kuzingatia jema na baya, kuheshimu wakubwa na wadogo na kutoa uamuzi ulio sahihi.
2. Kuainisha uwezo, sifa za Mwenyezi Mungu (S.W.T) pamoja na kuhifadhi na kueleza majina kumi matukufu ya Mwenyezi Mungu.
3. Kuelezea sira ya Mtume Muhammad (S.AW) mpaka kupewa Utume.
4. Kusoma na kuhifadhi sura za Qur-an na hadithi za Mtume (S.A.W) zilizochaguliwa.
5. Kuelezea maana ya tohara.
6. Kujitoharisha, kutia udhu na kusali.

## Malengo ya Jumla ya Somo la Dini

Somo la Dini linafundishwa katika skuli za Maandalizi ili watoto waweze:

1. Kujenga tabia njema na kufuata utaratibu mzuri wa kuishi katika jamii kwa kujua jema na baya, kuheshimu wakubwa na wadogo na kuweza kutoa uamuzi ulio sahihi.
2. Kutambua na kuthamini uwezo wa Mwenyezi Mungu (S.W.T) na kuweza kuhifadhi na kuelezea majina yake kumi (10) matukufu.
3. Kutambua sira ya Mtume Muhammad (S.A.W) mpaka kupewa Utume.
4. Kupata stadi za uhifadhi wa sura za Kur – an na hadithi za Mtume (S.A.W) zilizochaguliwa.
5. Kuelewa maana ya tohara.
6. Kujua namna ya kujitoharisha, kutia udhu na kusali.

# MUHTASARI WA DINI KWA MWAKA WA KWANZA

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 1. TABIA<br>(a) Tabia | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja tabia njema | Kwa kutumia mbinu ya hadithi, mwalimu awaongoze watoto kusikiliza hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W) zenye kuelezea tabia njema | 1. Chati za hadithi<br>2. Redio<br>3. CD<br>4. Chati mguso | 3 |
| | (ii) Kuonesha mifano ya tabia njema kwa vitendo. | Kwa kutumia igizo mwalimu awaongoze watoto kuonesha tabia njema kwa vitendo mfano upendo, uaminifu, ukweli nk. | 1. Chati za hadithi<br>2. Redio<br>3. CD<br>4. Chati mguso | |
| (b) Heshima | Mtoto aweze Kuwaheshimu wakubwa na wadogo.. | Kwa kutumia mbinu ya igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza yafuatayo<br>- Kusalimiana (kuamkiana)<br>- Kupokea mzigo.<br>- Kuwasaidia wenye mahitaji maalumu ya kielimu n.k | 1. Vitu halisi.<br>2. Chati zinazoendana na mada<br>3. Chati mguso | 2 |
| | | - Kufanyia wema wazazi wawili<br>- Ihsani kwa wanyama | | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| (c) Kanuni | Mtoto aweze Kuzitumia kanuni mbali mbali. | Kwa kutumia mbinu ya igizo, mwalimu awaongoze watoto kuigiza igizo litakalowawezesha kutumia maneno ahsante anapopewa kitu, samahani anapokosea, tafadhali anapoomba kitu. | Vitu halisi | 3 |
| 2. SIRA<br>(a) Maisha ya Mtume Muhammad (S.A.W) | Mtoto aweze:-<br>Kutaja jina , tarehe na pahala alipozaliwa Mtume Muhammad (S.A.W) | 1. Kwa kutumia mbinu ya kasida mwalimu awaongoze watoto kukariri jina, tarehe na pahala alipozaliwa Mtume Muhammad (S.AW).<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kukariri mwalimu awasisitize watoto kusema (S.A.W) | 1. Kaseti za kasida.<br>2. CD.<br>3. Kadi za jina.<br>4. Picha za Msikiti wa Makka (Alkaaba) | 3 |
| | | linapotajwa jina la Mtume Muhammad (S.A.W) | | |
| (b) Watoto wa Mtume Muhammad (S.A.W) | Mtoto aweze<br>Kutaja idadi ya watoto wa Mtume Muhammad (S.A.W) pamoja na majina yao, Idadi | Kwa kutumia mbinu ya kasida , mwalimu awaongoze watoto kutaja idadi ya watoto wa Mtume (S.A.W) pamoja na majina yao | 1. Chati ya majina<br>2. Chati mguso<br>3. Kaseti za | 2 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | yao na mgawanyo wa kijinsia. | | kasida na CD | |
| (c) Sifa za Mtume Muhammad (S.A.W) | Mtoto aweze:<br>Kutaja sifa za Mtume (S.A.W) pamoja na kuzifuata kwa vitendo. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kisa mafunzo, mwalimu awaongoze watoto kusikiliza visa na hadithi za Mtume (S.A.W) zinazotaja sifa zake.<br>2. Kwa kutumia igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza michezo inayoonesha sifa za Mtume (S.A.W).na kuzitumia kwa vitendo | 1. CD<br>2. Kasida.<br>3. Redio<br>4. Vitu halisi. | 2 |
| 3. KUR'AN<br>(a) Suratul fatha.<br>Suratul nnas<br>Suratul falaq<br>Suratul Ikhas | Mtoto aweze:-<br>(i) Kusoma sura kwa usahihi. | Kwa kutumia onyesho mbinu, mwalimu awaongoze watoto hatua kwa hatua kusoma sura kwa usahihi. | 1. Maandishi ya Braille.<br>2. Chati za sura.<br>3. Kaseti.<br>4. Chati mguso za sura.<br>5. Juzuu ya Amma. | 3 |
| | (ii) Kusoma na kuhifadhi. | Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudiarudia, mwalimu | 1. Maandishi ya Braille | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | awaongoze watoto hatua kwa hatua kusoma sura kwa usahihi na kuzihifadhi. | 2. Chati za sura.<br>3. Kaseti.<br>4. Chati mguso za sura. | |
| 4. HADITHI<br>(a) Kusoma Hadithi ya Usafi | Mtoto aweze:-<br>Kuhifadhi hadithi kwa usahihi. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudiarudia mwalimu awaongoze | 1 Chati za hadithi<br>2. Chati mguso | 6 |
| Hadithi ya Upendo<br>Adabu za Kula<br>Kupeana Zawadi<br>Adabu za Kunywa | | watoto hatua kwa hatua kuhifadhi hadithi kwa usahihi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya igizo mwalimu awaongoze watoto kuhifadhi hadithi kwa usahihi. | | |
| 5. TAWHIDI<br>(a) Uislamu | Mtoto aweze:-<br>(i) Kuelezea maana ya utukufu wa uislam kwa ufupi | Kwa kutumia mbinu ya kasida mwalimu awaongoze watoto kuelezea maana ya uislamu kwa ufupi. | 1. Kaseti za kasida<br>2. CD<br>3. Chati ya nguzo za kiislam | 3 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kuelezea heshima na ukarimu wa uislamu | Kwa kutumia mbinu ya kisa mafunzo mwalimu awaongoze watoto kusikiliza visa mbali mbali pamoja na | 1. CD.<br>2. Redio.<br>3. Kanda za sauti. | |
| | | hadithi za Mtume (S.A.W) zinazoelezea heshima na ukarimu wa uislamu. | | |
| (b) Nguzo za Uislamu | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja nguzo za uislamu kwa mtiririko. | Kwa kutumia mbinu ya kasida mwalimu awaongoze watoto kutaja nguzo za uislam kwa mtiririko. | 1. Chati ya nguzo za kiislamu/chati mguso<br>2. CD.<br>3. Redio<br>4. Kanda za sauti. | 3 |
| | (ii) Kuelezea nguzo za uislam. | Kwa kutumia mbinu ya igizo mwalimu awaongoze watoto kuelezea nguzo za uislam. | 1. Chati ya nguzo za uislamu/Chati mguso.<br>2. CD.<br>3. Redio/<br>4. Kanda za sauti. | |
| (c) Majina ya Mwenyezi | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja majina ya | Kwa kutumia mbinu ya kasida mwalimu awaongoze watoto | 1. Kaseti<br>2. CD | 2 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| Mungu. | Mwenyezi Mungu | kusoma kasida ya majina ya M/Mungu kwa usahihi. | | |
| | (ii) Kupanga kadi za majina ya M/Mungu | Kwa kutumia mbinu ya mchezo mwalimu awaongoze watoto kupanga kadi za majina ya M/Mungu kwa mtiririko. | Kadi za majina ya M/Mungu | |
| 6. IBADA<br>(a) Najisi | Mtoto aweze:-<br>(i) Kueleza maana ya najisi kwa ufupi | 1. Kwa kutumia mhadhara mfupi mwalimu awaongoze watoto kueleza maana ya najisi.<br>2. Kwa kutumia mazoezi ya kurudia rudia mwalimu awaongoze watoto kukariri maana ya najisi. | 1. Maji.<br>2. Kata.<br>3. Vijiwe<br>4. Chati/chati mguso | 4 |
| | (ii) Kuepuka kuchezea najisi | Kwa kutumia mbinu ya igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza mchezo unaoonesha madhara ya kuchezea najisi. | 1. Maji.<br>2. Kata.<br>3. Vijiwe.<br>4. Chati/chati mguso | |
| (b) Udhu | Mtoto aweze:- | 1. Kwa kutumia onesho mbinu | 1. Maji. | 2 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | Kutia udhu kamili kwa vitendo na kwa usahihi | mwalimu awaongoze watoto kutia udhu kamili kwa vitendo.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana mwalimu awaongoze watoto kufundishana kutia udhu kwa usahihi. | 2. Kata.<br>3. Kopo<br>4. Chati ya kutia udhu/chati mguso | |
| (c) Sala. | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja vipindi vya sala. | Kwa kutumia mbinu ya kasida mwalimu awaongoze watoto kutaja vipindi vya sala. | Chati ya watu wanaosali/chati mguso | 3 |
| | (ii) Kusali kwa vitendo | Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano mwalimu awaongoze watoto kusali kwa vitendo. | Chati ya watu wanaosali/chati mguso | |
| (d) Dua. | Mtoto aweze:-<br>Kusoma dua ndogo ndogo,. | 1. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto hatua kwa hatua kusoma dua kwa usahihi (dua ya kuingia na kutoka chooni , | Chati za dua/chati mguso. | 3 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | kuanza kula na kumaliza kula n.k.<br>2. Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto kusoma dua za wakati wa kulala na kuamka na duwa wakati wa kwenda chafya | | |

## MWAKA WA PILI

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| 1. TABIA<br>(a) Tabia | Mtoto aweze<br>Kutofautisha tabia njema na mbaya. | 1. Kwa kutumia mbinu ya igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza mchezo wenye kuonesha tabia tofauti.<br>2. Kwa kutumia maswali na majibu mwalimu awaongoze watoto kutofautisha tabia njema na mbaya kutokana na igizo. | Vitu halisi | 2 |
| (b) Heshima kwa Wakubwa na Wadogo | Mtoto aweze<br>Kuwaheshimu wakubwa na wadogo wake, | Kwa kutumia mbinu ya kisa, mafunzo mwalimu awaongoze watoto kusikiliza visa mbali mbali vinavyoonesha ubaya wa kutowaheshimu wakubwa na wadogo. | Vitu halisi | 2 |
| (c) Kanuni | Mtoto aweze<br>Kutumia kanuni mbali mbali. | Kwa kutumia igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza igizo itakalowawezesha kutumia maneno Ahsante anapopewa | Vitu halisi. | 2 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | kitu, samahani anapokosea , tafadhali tafadhali anapoomba. | | |
| 2. TABIA<br>(a) Kuheshimu Mawazo ya Wengine. | Mtoto aweze<br>Kuheshimu mawazo ya wengine, kuonesha namna ya kuheshimu mawazo | Kwa kutumia mbinu ya igizo mwalimu awaongoze watoto kuigiza mchezo utakaonesha umuhimu wa kuheshimu mawazo ya wengine. | Vitu halisi | 2. |
| 3. SIRA<br>(a) Ujana wa Mtume (S.A.W). | Mtoto aweze<br>Kueleza tabia za Mtume (S.A.W) katika ujana wake. | Kwa kutumia mbinu ya kasida mwalimu awaongoze watoto kutaja tabia na sifa za Mtume katika ujana wake. | 1. Kaseti.<br>2. CD.<br>3. Chati inayoonesha wanyama aliokuwa akichunga bidhaa alizosafirisha | 2 |
| (b) Wake wa Mtume Muhammad (S.A.W) | Mtoto aweze<br>(i) Kutaja idadi ya wake wa Mtume (S.A.W) pamoja na majina yao. | 1. Kwa kutumia mbinu ya kasida mwalimu awaongoze watoto kukariri idadi ya wake wa Mtume (S.A.W) pamoja na majina yao.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kucheza mwalimu awaongoze watoto kucheza | 1. CD.<br>2. Redio.<br>3. Kanda za sauti.<br>4. Kadi za majina<br>5. Kadi zenye maandishi ya Braille. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | michezo mbali mbali kwa kutumia kadi za majina ya wake wa Mtume (S.A.W). | | |
| (c) Mitume 25 | Mtoto aweze<br>Kutaja majina ya Mitume. 25 waliotajwa katika kur –ani kwa mtiririko wake | Kwa kutumia mbinu ya kasida mwalimu awaongoze watoto kutaja idadi ya Mitume iliyotajwa katika Kur –ani na kutaja majina ya | 1. Chati ya majina | 4 |
| | | Mitume kwa mtiririko wake.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia mwalimu awaongoze watoto kukariri majina ya Mitume 25 iliyotajwa katika kur –ani kwa mtiririko wake. | 2. Kaseti<br>3. CD.<br>4. Chati mguso<br>5. Kadi za majina<br>6. Redio | |
| 4. KUR - ANI<br>(a) Suratui Lahab, Nasir, Kafirun na Kawthar. | Mtoto aweze<br>(i) Kusoma sura kwa usahihi. | Kwa kutumia onesho mbinu mwalimu awaongoze watoto hatua kwa hatua kusoma kwa usahihi. | 1. Chati za sura.<br>2. Chati mguso.<br>3. Kaseti<br>4. Juzuu ya Amma .<br>5. CD. | 6 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | (ii) Kusoma na kuhifadhi. | Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia mwalimu awaongoze watoto hatua kwa hatua kusoma na kuhifadhi sura kwa usahihi. | 1. Chati za sura.<br>2. Chati mguso.<br>3. Kaseti<br>4. Juzuu ya Amma<br>5. CD. | |
| 6. HADITHI<br>(a) Kusoma na Kutafsiri Hadithi<br>Sifa za Mnafiki.<br>Ukamilifu Wa Sala.<br>Miongoni mwa Sifa za Alla<br>Umuhimu wa Kusoma Kur - ani | Mtoto aweze<br>Kuhifadhi hadithi na tafsiri zake. | 1. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia mwalimu awaongoze watoto hatua kwa hatua kuhifadhi hadithi na tafsiri zake.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya igizo mwalimu awaongoze watoto kuhifadhi hadithi na tafsiri zake. | 1. Chati/Chati mguso za hadithi.<br>2. Redio.<br>3. kanda za sauti.<br>4. CD. | 7 |
| 6. TAWHID | Mtoto aweze | 1. Kwa kutumia mbinu ya | 1. Kadi za majina. | 5 |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| (a) Majina ya Mwenyezi Mungu. | Kutaja majina ya Mwenyezi Mungu. | kasida mwalimu awaongoze watoto kutaja majina ya M/Mungu kwa usahihi.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya mchezo mwalimu awaongoze watoto kupanga kadi za majina ya M/Mungu kwa usahihi<br>3. Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia mwalimu awaongoze watoto hatua kwa hatua kukariri majina. | 2. Chati ya majina ya M/Mungu/ Chati mguso | |
| (b) Nguzo za Imani | Mtoto aweze\|<br>(i) Kutaja idadi ya nguzo za imani. | Kwa kutumia mbinu ya kasida mwalimu awaongoze watoto kutaja idadi ya nguzo za imani. | 1. Chati ya nguzo za imani.<br>2. Chati mguso<br>3. Redio. | 2 |
| | (ii) Kutaja nguzo za imani kwa mtiririko. | Kwa kutumia mbinu ya mazoezi ya kurudia rudia mwalimu awaongoze watoto kukariri nguzo za imani kwa usahihi. | 1. Chati ya nguzo za imani.<br>2. Chati mguso<br>3. Redio. | |

| MADA KUU/MADA NDOGO | MALENGO MAHSUSI | MBINU ZA KUFUNDISHIA/ KUJIFUNZIA | VIFAA | VIPINDI |
|---|---|---|---|---|
| | | | 4. CD. | |
| 7. IBADA<br>(a) Udhu | Mtoto aweze<br>Kutia udhu kwa kufuata utaratibu | 1. Kwa kutumia mbinu ya igizo mfano mwalimu awaomgoze watoto kutia udhu kwa kufuata utaratibu.<br>2. Kwa kutumia mbinu ya kufundishana mwalimu awaomngoze watoto kufundisha kutia udhu kwa kufuata utaratibu | 1. Maji<br>2. Kata<br>3. Chati ya namna ya kutia udhu/chati mguso | 2 |
| (b) Sala | Mtoto aweze:-<br>(i) Kutaja vipindi pamoja na nyakati za sala. | Kwa kutumia mbinu ya kasida mwalimu awaongoze watoto kutaja vipindi na nyakati za sala. | 1. Kanga<br>2. Msala<br>3. Chati ya watu wanaosali/chati mguso | 2 |
| | (ii) Kusali kwa vitendo | Kwa kutumia igizo mfano mwalimu awaongoze watoto kusali kivitendo | 1. Kanga<br>2. Msala<br>3. Chati ya watu wanaosali | |